**TAARIFA YA MRADI WA KIWANDA CHA KUKOBOA NAFAKA UNAOTEKELEZWA NA CHAMA CH USHIRIKA KIMULI KATIKA KIJIJI CHA MTAMA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA NDUGU CHARLES FRANCIS KABEHO TAREHE 05-06-2018.**

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018,** Ninayo furaha kubwa kukukaribisha pamoja na Msafara wote uliofuatana nao hapa Kijiji cha Mtama nasema karibu sana na ujisikie upo nyumbani.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018,** Mradi wa kiwanda cha kukoboa nafaka ulianzishwa mwezi Disemba 2016. Madhumuni ya kuanzishwa kwa mradi huu ni kutoa huduma na kukiongezea chama mapato na kupata uzoefu wa kuanzisha kiwanda kikubwa kuunga mkono Sera ya kuendeleza Viwanda nchini kwa kuchakata nafaka ili kuongezea mnyororo wa thamani.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018,** Mpango wetu ni kuendeleza Mazao ya Nafaka katika Maeneo yetu kupitia chama chetu cha ushirika cha KIMULI kwa kuwawezesha wananchi kiutaalamu na Kiushauri.Kiwanda hiki ambacho unakizindua leo ndugu kiongozi wa mbio za mwenge kimegharimu kiasi cha Tshs **18,200,000/=** Gharama hizo ni pamoja na ujenzi wa jengo,ununuzi wa mashine na uingizaji umeme.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018,** Mradi huu una uwezo wa kuchakata kiasi cha kilo 5000 za nafaka kwa siku (kukoboa na kusaga).Mradi huu umefanikiwa kuajiri watu 2 wa kudumu. Lengo la chama ni kuanzisha miradi kama hii katika maeneo ambayo yatafikiwa na umeme .Licha ya mradi huu, chama cha msingi KIMULI kimewekeza katika sekta ya elimu kiasi cha Tshs Mil 45 ikiwa sehemu ya mchango wa kuwezesha jamii kupata elimu bora

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018,** Naamini ya kwamba Mafanikio ya Uchumi wa Viwanda yanategemea uzalishaji wa uhakika wa Mazao ya Kilimo,na wataalamu wenye weledi ikiwa ni matokeo ya uwekezaji thabiti kwenye elimu .Hivyo kuunga mkono kauli mbiu **'Elimu ni ufunguo wa Maisha ,Wekeza sasa kwa maendeleo ya Taifa letu'**.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018,** Nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuimarisha Ushirika nchini kwani kuimarika kwa ushirika kutainua Uchumi wa Wanachama na Wakulima wote kwa ujumla.Chama msingi KIMULI ni miongoni mwa vyama 14 vilivyopo katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018,** Tunaahidi kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuleta maendeleo kila tutakapokuwa na uwezo kama tunavyofanya.

Ni sisi Chama cha Ushirika KIMULI**.**

**KIMULI AMCOS**
**KIJIJI CHA MTAMA**
**KATA YA UTIRI**